

GRADE 4 END TERM 3 DECEMBER 2021

KISWAHILI ACTIVITIES

Jina

Jina la shule

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

Viwango vya kutathmini				
	Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
Kusikiliza na Kuzungumza	5 <input type="checkbox"/>	4 <input type="checkbox"/>	3 <input type="checkbox"/>	0 - 2 <input type="checkbox"/>
Kusoma kwa sauti	Maneno 71 na zaidi <input type="checkbox"/>	Maneno 51-70 <input type="checkbox"/>	Maneno 25 - 50 <input type="checkbox"/>	Maneno 0 - 24 <input type="checkbox"/>
Sarufi	19 - 20 <input type="checkbox"/>	13 - 18 <input type="checkbox"/>	6 - 12 <input type="checkbox"/>	0 - 5 <input type="checkbox"/>
Ufahamu	5 <input type="checkbox"/>	4 <input type="checkbox"/>	3 <input type="checkbox"/>	0 - 2 <input type="checkbox"/>

SEHEMU YA KWANZA

I. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

(alama 5)

Ninaitwa Bi/Bw _____ na ningependa tuzungumzie kuhusu bendera yetu. -

- Rangi za bendera ya Kenya ni ngapi? (alama 1) (Mwanafunzi ajibu)
- Rangi za bendera ya Kenya ni zipi? (alama 2) (Mwanafunzi ajibu)
- Sema kila rangi inaashiria nini. (alama 2) (Mwanafunzi ajibu)

II. KUSOMA KWA SAUTI.

Soma kifungu kifuatacho kwa sauti mwalimu akisikiliza. (alama 10)

Kemoi anaishi katika kijiji cha Tia Adabu. Yeye na dada yake Chebet wanapendana sana. Ni kawaida kwa Kemoi kuamka kabla ya Chebet. Anapoamka huchukua kiberiti na kuwasha taa ya kibatari. Kemoi anajua kukoka moto akitumia makumbi ya nazi. Yeye hujikaza kupika kahawa na kaimati ya kiamshakinywa. Baada ya kuoga, Kemoi huvaa suruali ya zambarau na sweta ya buluu.

III. SARUFI.

(Alama 20)

1. Andika sentensi hizi kwa wingi

(alama 3)

- a) Jasho lilimtiririka. _____
- b) Jua limechomoza. _____
- c) Giza limeingia. _____

2. Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

(alama 3)

- a) omba radhi _____
- b) toa shukrani _____
- c) piga hodi _____

3. Tumia "li" au "ya" kujaza pengo.

(alama 4)

- a) Godoro __menyeshewa.
- b) Madirisha __lifunguliwa.
- c) Soko __lijengwa upya.
- d) Madawati yote __mepanguswa

4. **Andika sentensi hizi kwa umoja.**

(alama 3)

a) Milango imefunguliwa. _____

b) Mizizi imeinuka juu. _____

c) Miche ilikauka. _____

5. **Kamilisha methali hizi.**

(alama 3)

a) Teke la kuku _____

b) Mtoto akibebwa hutazama _____

c) Mtoto umleavyo _____

6. **Andika maneno ya upole badala ya maneno yafuatayo.**

(alama 4)

a) Wanahara - _____

b) Amezaa - _____

c) Ana mimba - _____

d) Matakoto - _____

IV. **KUSOMA UFAHAMU.**

(alama 5)

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.

Yohana aliamka akiwa na furaha. Mjomba wake alikuwa amewapangia ziara. Ilikuwa ziara ya kutembelea mbuga ya wanyama ya Maasai Mara. Bwana Upendo, mjomba wake, alikuwa amekodi gari la kuwapeleka ziara hiyo.

Yohana alipoingia mjomba alipiga gari moto na safari ikaanza. Yohana na binamu zake Bidii na Rehema waliona vitu vingi safarini. Waliona magari, watu,

mashamba na pia waliona bonde kubwa. Bwana Upendo aliwaambia linaitwa Bonde la Ufa. Waliona Mlima Longonot ndani ya bonde lile. Baada ya kusafiri kwa muda walifika Maasai Mara. Walilipa pesa na kuingia ndani ya mbuga wakielekezwa na mlinzi.

a) Kwa nini Yohana aliamka akiwa na furaha? **(alama 1)**

b) Yohana aliandamana na akina nani safarini? **(alama 1)**

c) Taja baadhi ya vitu walivyoviona Yohana na binamu zake wakiwa safarini. **(alama 2)**

d) Yohana na binamu zake waliona bonde gani? **(alama 1)**

e) Walipofika Maasai Mara walifanya nini ili kuruhusiwa kuingia mbugani? **(alama 1)**
